

Kuna utaratibu fulani ambao ajenti au kabaila wafuate kama wakitaka kuzidisha kodi yako.

Unapoweka saini hati ya kukodisha – kawaida ni kwa kipindi cha miezi 6 au miezi 12.

Mnamo muda huu, kabaila hawezi kuzidisha kodi, isipokuwa inaandikwa katika hati ya kukodisha kwamba wanaruhusu kufanya hivyo.

Hati ya kukodisha ionyeshe kiasi au njia ya mahesabu ya ongezo.

Kabaila anaweza kuzidisha kodi kama mpangaji ana hati ya kukodisha kwa kipindi cha miaka 2 au zaidi.

Kama ukikubali mkataba yako ya kupangisha tena kwa kipindi kingine, kodi haiwezi kuzidishwa bila kufikiri

Wakati wote lazima ajenti au kabaila wakupe notisi ya siku 60 kabla ongezo linaweza kufanyikiwa.

Kwa mfano, kama mkataba yako ya kupangisha ni kwa miezi 6 au 12 na unaendelea bila kuweka saini kwa mkataba mpya, kodi inaweza kuongezwa kama unapata notisi ya siku 60 kwanza.

Kama huwezi kumudu kulipa kodi iliyozidishwa ongea na ajenti au kabaila yako mara moja. Wanaweza kukubali kwa ongezo dogo zaidi kama umekuwa mpangaji mzuri.

Kama wakikubali – hakikisha imeandikwa.

Kama ukifikiri ongezo la kodi ni kupita kiasi - waweza kuomba kwa Consumer, Trader and Tenancy Tribunal (Mahakama ya Mtumiaji, Mwenye biashara na Upangaji) kufanya amuzi kama ongezo ni kubwa mno.

### **Je, naweza kukodisha miliki na mpangaji mwingine?**

Wapangaji wengine wanataka kuokoa pesa kwa njia ya kugawa miliki na mtu mwingine.

Kama mpangaji anakodisha chumba ziada, gereji au ghorofa la bibi kwa mtu mwingine – hii inaitwa kukodisha nyumba iliyokodishwa.

Mtu mwingine anayepanga nawe anakuwa mpangaji wa kugawia.

Mpangaji anakusanya kodi kutoka mpangaji wa kugawia na ana jukumu pia kwa madhara yoyote yaliyofanywa na mpangaji wa kugawia.

Lazima wapangaji waombe ajenti au kabaila kabla ya kukodisha miliki.

Kabaila hawezi kukataa kukuruhusu kukodisha chumba kwa mtu mwingine – isipokuwa kuna sababu nzuri.

Lakini ukitaka kukodisha miliki mzima na kuhama ndipo kabaila anaweza kukataa. Pia anaweza kukataa akifikiri itasababisha tatizo kama kusongamana songa.

Kwa mfano, kama kuna watu 8 kuishi katika ghorofa au nyumba ya vyumba 2 vya kulala, kungekuwa watu wengi mno kuishi kwa mahali padogo. Hivi vinaonekana kusongamana songa.

Kama ukiamini kabaila yako asiye na haki kuhusu hiyo, waweza kuomba kwa Consumer, Trader and Tenancy Tribunal (Mahakama ya Mtumiaji, Mwenye biashara na Upangaji) kutatua jambo.

Mahakama yataamua ipi ni haki.

Kupata maelezo zaidi kuhusu haki na majukumu ya wapangaji, tembelea tovuti ya Fair Trading kwa [www.fairtrading.nsw.gov.au](http://www.fairtrading.nsw.gov.au) au piga simu namba ya 13 32 20.

Kama ukihitaji msaada wa lugha pigia simu 13 14 50.